# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# BARAZA LA MITIHANI
# MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A

**636** **TEHAMA**

**Muda: Saa 3.** **Mwaka: 2008**

---

**Maelekezo.**

1. Karatasi hii ina sehemu **A** na **B.**
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu **A** na maswali **manne (4)** kutoka sehemu **B**.
3. Zingatia maelekezo ya kila swali.
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Eleza maana ya mfumo wa uendeshaji kisha taja kazi zake kuu mbili.
2. Bainisha tofauti tatu kati ya zana za kufundishia zilizotengenezwa na mwalimu na zile za kununuliwa sokoni.
3. Fafanua umuhimu wa vitabu vya kiada katika kufundishia somo la TEHAMA.
4. Onyesha matumizi manne ya kifaa cha simu ya mkononi katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la TEHAMA.
5. Eleza kwa ufupi maana ya Makumbusho ya Taifa kisha taja umuhimu wake mmoja katika masomo.
6. Taja faida nne za mwalimu kutumia mfumo wa kuuliza maswali katika kipindi cha darasa.
7. Fafanua kanuni nne za usalama zinazotakiwa kufuatwa wakati wa kutumia zana za umeme darasani.
8. Ainisha aina tatu za upimaji wa uwezo wa mwanafunzi kulingana na muda wa kufanya upimaji.
9. Bainisha hatua tano zinazotakiwa kufuatwa wakati wa kuandaa maonesho ya Bango kwa ajili ya darasa la TEHAMA.
10. Eleza kwa kifupi maana ya mawanda ya ujifunzaji kisha toa mfano mmoja wa kila wanda.

## SEHEMU B (Alama 60)

Jibu maswali **manne (4)** kutoka katika sehemu hii.

11. Eleza kwa kutoa hoja tano umuhimu wa mwalimu wa TEHAMA kujua namna ya kutengeneza zana za kufundishia.
12. Tathmini kwa kutoa hoja tano namna mawasiliano ya kimaandishi yanavyoweza kutumika kwa ufanisi katika ufundishaji wa somo la TEHAMA.
13. Fafanua mambo matano yanayoweza kuathiri ufaafu wa matokeo ya mitihani ya wanafunzi katika somo la TEHAMA.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

14. Chunguza vigezo vitano vinavyoweza kutumika kutathmini ufaafu wa kitabu cha kiada cha somo la TEHAMA.

15. Eleza namna mwalimu wa TEHAMA anavyoweza kutumia zana za michezo katika kufundishia stadi za Kompyuta.

16. Bainisha kanuni tano za kutunga jaribio au mtihani unaohusisha maswali ya kujaza nafasi zilizo wazi.

17. Fafanua mambo matano yanayoweza kumfanya mwalimu kubadili mbinu za kufundishia katikati ya somo.

18. Eleza dhima tano za kufundishia wanafunzi namna ya kutumia barua pepe kwa usahihi na usalama.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org